# HOTUBA YA MGENI RASMI MHE AMINA JUMA MASENZA MKUU WA MKOA WA IRINGA KWENYE MAADHIMISHO YA KILELE CHA WIKI LA KUSOMA NGAZI YA MKOA TAREHE 25/05/2017 KATIKA UWANJA WA MASHUJAA MJINI MAFINGA

Katibu Tawala Mkoa wa Iringa,

Waheshimiwa Wakuu wa Wilaya mliohudhuria,

Mhe. Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi Wilaya,

Ndugu viongozi wa Madhehebu ya Dini,

Makatibu Tawala Wasaidizi Mkoa,

Wah. Wenyeviti Halmashauri za Mkoa wa Iringa,

Wah. Wenyeviti wa Kamati za Huduma za Jamii wa Halmashauri za Mkoa wa Iringa,

Wakurugenzi wa Halmashauri za Mkoa wa Iringa,

Wataalamu wa Elimu Sekretarieti ya Mkoa wa Iringa,

Maafisa Elimu Msingi na Sekondari (W),

Mwenyekiti na Katibu wa Chama cha Walimu (W),

Wakuu wa Vyuo na Taasisi mbalimbali za Serikali, Wakuu wa Shule Msingi na Sekondari,

Walimu,

wanafunzi,

Wageni Waalikwa,

Waandishi wa Habari,

Mabibi na Mabwana.

Awali ya yote napenda kutumia fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kufika hapa kwa ajili ya maadhimisho ya Wiki la kusoma katika Mkoa wetu wa Iringa. Binafsi nimefurahi sana kupata fursa ya kushiriki maadhimisho haya ambayo yanalenga kukuza na kuongeza ari ya ushindani katika kujifunza stadi za msingi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK). Kupitia mkusanyiko huu unaojumuisha wadau mbalimbali wa Elimu ni fursa ya kushirikishana namna ya kutatua changamoto katika mchakato mzima wa utoaji wa Elimu bora kwa watoto wetu.

Ninachukua fursa hii pia kuwashukuru wenyeji wetu, Halmashauri ya Mji Mafinga kwa kukubali kuwa wenyeji wa maadhimisho haya Kimkoa. Shukrani zangu ziwaendee viongozi na wananchi wote wa Halmashauri za Wilaya katika Mkoa wa Iringa kwa mwitikio na ushiriki wenu kwa namna moja au nyingine katika kufanikisha maandalizi na hatimaye maadhimisho ya siku hii. Mwisho nawashukuru watumishi mbalimbali kutoka katika Ofisi yangu kwa kuratibu vema shughuli zote zinazohusiana na maadhimisho haya.

Ndugu Wananchi,

Wiki la kusoma kwa Mkoa wa IRINGA lilianza tarehe 19/05/2017 na linahitimishwa kimkoa leo tarehe 25/05/2017 katika Halmashauri ya Mji wa MAFINGA ambapo Halmashauri zote za Mkoa wa Iringa zimeshiriki kikamilifu baada ya kuwa zimefanya maadhimisho hayo katika ngazi ya Halmashauri.

Maadhimisho ya Wiki la kusoma kwa mwaka 2017 yanakusudia kutumika kutoa msukumo mpya katika kuendeleza elimu hasa uimarishaji wa umahiri wa misingi ya Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK). Kaulimbiu yetu mwaka huu inasema: "Ufundishaji bora wa stadi za kusoma, kuandika na kuhesabu ni msingi wa maarifa, ujuzi na maendeleo ya elimu katika kufikia uchumi wa viwanda".

Ninatoa pongezi za dhati kwa wote waliofanikisha maadhimisho haya na wanafunzi wote walioshiriki na kuonesha ushindani. Kazi hii iwe chachu ya kupiga hatua kubwa zaidi katika kufikia malengo ya Serikali yetu ya awamu ya tano ya kuwa na uchumi wa viwanda. Dhamira na juhudi mbalimbali zinazofanywa na Serikali yetu ni kuhakikisha kuwa ubora wa elimu tunayoitoa unaanza na uimarishaji wa misingi ya stadi za KKK.

Ndugu Wananchi,

Serikali yetu ya Awamu ya Tano chini ya Uongozi wa Rais Mhe. Dr. John Pombe Magufuli inafanya juhudi za dhati za kuhakikisha kuwa elimu inaboreshwa na kuondoa baadhi ya michango isiyo ya lazima kwa utekelezaji wa mpango wa Elimu bila Malipo. Ni dhahiri kuwa Serikali yetu inastahili pongezi za dhati kwa kutekeleza kwa umakini Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya kutoa Elimu bila malipo. Katika kufanikisha haya Serikali inashirikiana na Mashirika ya kitaifa na kimataifa kufanikisha kazi hii. Serikali kwa kushirikiana na wafadhili tumefanikiwa kujenga uwezo kwa watendaji

wetu katika ngazi ya elimu. Ninawashukuru sana wafadhili wote tunaoendelea kushirikiana na ninaomba tuendeleze ushirikiano huo.

Ndugu Wananchi,

Mafanikio ya maadhimisho haya ni matunda ya kila mmoja kutekeleza wajibu wake katika nafasi yake ama kwa mchango wa mawazo au kubuni mikakati ya kufikia mafanikio tunayoyaona leo. Pongezi kwenu viongozi katika sekta ya elimu na wadau wote ambao mmefanikiwa kuufikisha Mkoa katika mafanikio haya. Sote tumesikia kwenye Taarifa kuwa Mkoa wa Iringa tumeshika nafasi ya Tatu kitaifa kwa mtihani wa kumaliza Darasa la saba mwaka 2016 vilevile, nafasi ya Pili kitaifa kwa mtihani wa kumaliza kidato cha Nne Mwaka 2016. Ninatambua mafanikio haya yanatokana na ushirikiano baina yetu katika utekelezaji wa mikakati ya kutoa elimu bora kwa wanafunzi wetu.

Kwa pamoja ninawasihi tuendelee na moyo huu wa kujituma na kujitolea kwa maslahi ya Taifa letu. Kamwe tusibweteke na mafanikio tuliyoyapata bali tubaki na lengo la kushika nafasi ya kwanza kitaifa sambamba na kufaulisha kwa viwango vya juu zaidi. Tutumie fursa ya maadhimisho haya kutafakari mipango na mikakati ya kuboresha zaidi elimu katika Mkoa wetu. Lazima tujiwekee mipango ya utekelezaji inayopimika. Tutafakari mafanikio na mapungufu yaliyojitokeza katika ufaulu kwa mitihani ya ndani na nje na kuchukua hatua za kurekebisha mapungufu hayo.

Ndugu Wananchi,

Sote tumepata fursa ya kutembelea mabanda ya maonesho na kuona kazi nzuri zinazofanywa na wataalamu wetu katika Sekta ya Elimu. Tumejionea namna walimu wanavyotumia juhudi binafsi kuhakikisha wanafunzi wanamudu stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu ambazo ndiyo msingi wa Maendeleo ya elimu. Ni imani yangu kuwa kupitia maonesho hayo wengi tumejifunza juhudi zinazofanyika kuhakikisha wanafunzi wanamudu stati za kusoma, kuandika na kuhesabu. Ninaomba wazazi, walezi na wadau wote tuendelee kushirikiana ili kazi hii iwe endelevu.

Ndugu Wananchi,

Baada ya Serikali ya awamu ya Tano kuanza kutekeleza mpango wa elimu bila malipo kupitia Waraka wa Elimu Na. 6 wa Mwaka 2015,amabo umebainisha wazi majukumu ya kila mdau wa Elimu kama vile Serikali, Wazazi/Walezi, Walimu, Kamati/Bodi za shule na Jamii kwa ujumla kumejitokeza changamoto kadhaa. Pamoja na Waraka huo kubainisha majukumu ya Wadau, wapo watu wenye nia mbaya wanaopandikiza tafsiri potofu kuhusiana na utekelezaji wa mpango huo, hali inayosababisha baadhi ya wazazi na wana jamii kutotekeleza wajibu wao wakiamini kuwa hiyo ni kazi ya Serikali pekee.

Nichukue nafasi hii kuwaelekeza wataalam wa wa ngazi ya Mkoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa Mkoani Iringa kuweka mikakati ya kuhakikisha dhana ya elimu bila malipo kwa mujibu wa Waraka wa Elimu Na. 6 wa mwaka 2015 inaeleweka vizuri kwa wananchi wote ili waweze kushiriki kikamilifu katika kuchangia na kukuza Elimu katika Mkoa wa Iringa kwa sababu mafanikio yetu yatatokana na kujenga uelewa wa pamoja.

Ndugu Wananchi,

Tunao wajibu wa kuhamasisha wazazi/walezi kuwaandikisha shule watoto wote wenye umri lengwa, kutoa ushirikiano kwa wazazi/walezi ili kuhakikisha kuwa wanafunzi wanahudhuria shule wakati wote wa masomo, kutoa ushirikiano katika shughuli zote za kuleta maendeleo ya kielimu na kuendelea kujitolea nguvu na mali ili kuleta ustawi na maendeleo ya shule zilizoko katika jamii husika. Nimefurahi sana kuona namna mlivyojenga moyo wa ushindani na kupata Washindi wa zana za kufundishia na matumizi yake. Ufundishaji kwa kutumia zana za kufundishia ni muhimu sana katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji kwa mtoto.

Matumizi ya zana za kufundishia humfanya mwanafunzi kujenga uelewa na kumbukumbu ya kudumu katika jambo alilojifunza. Hivyo Mwalimu bora ni yule anayejiandaa vema na kuwa na zana za kufundishia zenye sifa stahiki.

Ndugu Wananchi,

Nichukue nafasi hii kuwapongeza wale wote waliofanikiwa kupata zawadi kutokana na ushindi katika maeneo mbalimbali ya ushindani katika maonesho haya. Ushindi huu ukawe chachu ya kuongeza juhudi na ubunifu katika kufikia mafanikio zaidi.

Ndugu Wananchi,

Mchango wa wadau na wafadhili mbalimbali umekuwa muhimu sana katika kukuza kiwango cha elimu katika Mkoa wa Iringa. Nachukua nafasi hii kuwashukuru sana wadau na wafadhiri wote kwa kuchangia Sekta ya Elimu Mkoani Iringa. Ni matumaini yangu kuwa mtaendelea kuunga mkono juhudi za Serikali za kuendeleza Sekta ya Elimu. Mniruhusu niwataje wafadhili watatu tu ambao watakuwa wamewakilisha wengine wote katika kuunga mkono juhudi za Serikali.

Wafadhili hao ni:-

1. Shirika la Kimataifa la Elimu (Global Partnership for Education-GPE), ambao wamewezesha Serikali kutekeleza mpngo wa kuongeza stadi za KKK kupitia program iitwayo LANES

2. Shirika la Kimataifa la misaada la Marekani (USAID)- ambao wamewezesha Serikali kutekeleza mpango wa kuongeza stadi za KKK kupitia program iitwayo – TUSOME PAMOJA inayo tekelezwa kwa ushirikiano na Taasisi ya RTI (Research Triangle Insitute – Tusome Pamoja).

3. Shirika la kuhudumia watoto Duniani (UNICEF) ambao pia wamewezesha Serikali kutekeleza mpango wa KKK kwa kutoa mafunzo kwa walimu mwaka 2014/2015 na sasa wanaendelea kuwwezesha Mkoa kuendesha shule shikizi (Satellite Schools).

Mwisho ninawapongeza tena wale wote walioshiriki kwa namna moja au nyingine kufanikisha maandalizi ya kilele cha maadhimisho ya Wiki ya Elimu Mkoa wa Iringa. Ni imani yangu kila mmoja atatoka na ari ya mabadiliko chanya na kwenda kuonesha utekelezaji wa kiwango cha juu katika shule, kata, Halmashauri na Mkoa kwa ujumla ili kuinua zaidi kiwango cha taaluma katika Mkoa wetu na Taifa kwa ujumla.

Ahsanteni kwa kunisikiliza